BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 25 Februari, 2025.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ya mwaka 2024/2025.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

171. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Je, ni ipi nafasi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika suala zima la usimamizi wa mazingira.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

190. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na utaratibu usioridhisha na unaolalamikiwa na wananchi walio wengi wa kuvitoza ada ya Shilingi 1,000/- vyombo vyote vya moto vinavyoingia katika Miji ya Mkoani na Chake Chake bila ya kuwa na maelezo yanayoridhisha.

(a) Je, ni vyombo vya aina gani vinalazimika kulipishwa ada ya Shilingi 1,000/- vinapoingia Miji ya Mkoani na Chake Chake.

(b) Je, tozo hii inadaiwa kwa mujibu wa sheria ipi na inaingia katika fungu lipi la bajeti.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

47. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kiasi gani mifumo ya TEHAMA iliyopo inasaidia kuwarahisisishia wawekezaji mbali mbali na kuwajengea mazingira wezeshi ya kufungua miradi yao hapa nchini.

81. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kuna baadhi ya maeneo ya uwekezaji hapa Zanzibar, bado hayawanufaishi wananchi kinyume na ahadi ya Serikali yao kwao kuwa, wanapokuwepo wawekezaji na huduma za kijamii pamoja na wananchi hunufaika kwa kiwango kikubwa.

Je, Serikali inatumia mbinu gani kurejesha imani ya wananchi ambao wanaamini hawanufaiki na baaadhi ya wawekezaji waliopo karibu na maeneo yao.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

169. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

   Je, kwa kiasi gani maendeleo ya sayansi na teknolojia yanachangia kuwepo kwa mifumo bora ya utoaji wa huduma za kibenki kwa haraka na usalama zaidi.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

42. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

   Wizara yako inatumia utaratibu gani wa kutathmini ubora wa huduma za kitalii zinazotolewa, ili kuhakikisha viwango vya juu vya kimataifa vya utoaji wa huduma za kitalii vinazingatiwa ipasavyo.

93. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

   Ni yepi malengo ya sera mpya ya utalii katika dhana ya kuwanufaisha wazawa.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

14. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

   Eneo la bandarini Wete limekuwa ni sehemu muhimu kwa popo (flying fox) wengi ambao wamekuwa wakilitumia eneo hilo kama sehemu ya kupumzika kupitia miti mikubwa inayopatikana katika eneo hilo. Hata hivyo, kuna tetesi kwamba popo hawa wameanza kupungua kwa kasi kubwa.

   (a) Je, tafiti zinaonesha nini kuhusu wingi na uzalishaji wa popo hao katika eneo hilo.

(b) Ni juhudi gani Serikali inafanya ili kuwalinda popo hawa ambao wapo katika orodha ya wanyama walio katika hatari ya kupotea.

(c) Je, Serikali inawatumia vipi popo hao ili waweze kuleta tija kwa wananchi na nchi kwa ujumla.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

117. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kivipi na kwa taratibu zipi Wizara yako inashughulika na suala zima la utoaji wa taarifa potofu kupitia vyombo mbali mbali vya habari nchini.

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kila ifikapo Julai 7 hutumiwa kama siku ya kimataifa ya kuadhimisha na kusherehekea siku ya Kiswahili duniani.

Je, tathmini iko vipi juu ya mafanikio ya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani kwa mara ya tatu hivi sasa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

182. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na kuimarika matokeo ya wanafunzi katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba. Hata hivyo, hakuna mabadiliko makubwa kwa matokeo ya wanafunzi wa kujitegemea (private candidates).

(a) Je, ni vigezo vipi kwa sasa vinatumika kuwaruhusu wanafunzi wa kujitegemea kufanya mitihani ya Taifa katika vituo na skuli za Unguja na Pemba.

(b) Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inaimarisha matokeo ya wanafunzi wanaojitegemea (private candidates) katika vituo na skuli za Unguja na Pemba.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

75. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika kujipatia ajira, wananchi wengi wa jimbo la Paje wanajiendeleza na kilimo cha mboga mboga, huku zao la ndimu likiwa ni zao kuu la biashara.

(a) Je, ni lini wananchi wa Jambiani watapatiwa umeme katika mashamba yao.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika unapatikana katika maeneo yote ya wakulima wa jimbo la Paje.

(c) Je, ni upi utayari wako wa kukutana na wananchi hao ili kuwapa moyo na uhakika wa kuzitekeleza ahadi za Wizara yako.

**Wizara ya Afya:**

70. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa Zanzibar. Mfuko huu una lengo la kuwapatia wananchi kwa visiwa vya Unguja na Pemba huduma za kinga na tiba zilizo bora kabisa. Na kwa kuwa muda mrefu sasa wananchi ambao tayari wamesajiliwa kujiunga na Mfuko huu, wameshapatiwa kadi za uwanachama wao wenyewe pamoja na wategemezi wao.

(a) Je, ni changamoto gani zinazoukabili Mfuko huu zinazosababisha kadi za wanachama kufungiwa mara kwa mara hali inayowapekelekea wanachama hao kushindwa kupata huduma.

(b) Kuna baadhi ya wanachama ambao tayari wameshasajiliwa na wameshahakikiwa kwa muda mrefu sasa lakini bado hawajazipata kadi zao (kadi ngumu) za uwanachama. Je, ni zipi hasa sababu zinazopelekea hali hii.

178. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ahadi inayohusiana na ujenzi wa vituo vipya vya afya vya Kiungoni na Pandani zimekuwa za muda mrefu. Hata hivyo, bado huduma katika vituo hivyo ni za kiwango cha chini.

(a) Je, ni hatua zipi tayari zimekamilika kuhusiana na ujenzi wa vituo vipya vya Kiungoni na Pandani.

(b) Kwa mujibu wa mpango wa Serikali, je,ni lini ujenzi wa vituo hivyo vipya unatarajiwa kukamilika na vitakuwa vituo vya hadhi gani.

(c) Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohudumiwa na vituo hivi, ni upi mpango wa dharura wa kutoa huduma bora wakati vituo vipya vikisubiri kujengwa.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ya mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**25 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**